



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI
OFISI YA MKURUGENZI WA HUDUMA ZA WANAFUNZI



TANGAZO KWA WANAFUNZI WAPYA WA SHAHADA YA KWANZA 2026/2027

Karibuni MUHAS - Kampasi ya Mloganzila!

Uongozi wa MUHAS unawapongeza na kuwakaribisha wanafunzi wote wapya waliochaguliwa kujiunga na programu mbalimbali za Shahada ya Kwanza kwa mwaka wa masomo 2026/2027.

Taarifa Muhimu

- 1. Maandalizi ya Kuwasili Chuoni:** Wanafunzi wote wanashauriwa kusoma kwa makini *Joining Instructions* walizotumiwa, kuandaa nakala halisi (*original copies*) za nyaraka zote muhimu za usajili na kufuatilia matangazo rasmi kupitia tofuvi ya MUHAS (www.muhas.ac.tz) kuhusu tarehe ya kuripoti na taratibu za usajili.
- 2. Malipo ya Ada na Gharama Nyingine:** Malipo yote ya ada (*tuition fees*) na gharama nyingine rasmi za chuo (*administrative fees*) yatafanyika kupitia **Namba za Malipo (Control Number) za Serikali** zitakazotolewa kwenye ankara (*invoices*) rasmi atakazopata mwanafunzi kupitia mfumo wa *Students Academic Records Information System* (SARIS) kupitia tovuti <https://saris2.muhas.ac.tz/login>. Maelezo zaidi ya matumizi ya SARIS yatatolewa kampasi ya Mloganzila wakati wa usajili tarehe **2 Novemba 2026**. Baada ya kufanya malipo, wanafunzi watatakiwa kuwasilisha risiti ya malipo chuoni. Wanafunzi wanatahadharishwa kuepuka kufanya malipo kwa watu binafsi au kutumia namba za malipo zisizo rasmi.

3. **Makazi ya Wanafunzi:** Chuo kina nafasi chache za malazi ndani ya kampasi ya Mloganzila ambazo zimetengwa kwa ajili ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza, kipaumbele ikiwa kwa wenye mahitaji maalumu kwa kuzingatia utaratibu na vigezo vilivyowekwa. Maombi ya makazi ndani ya kampasi yawasilishwe kupitia mfumo wa SARIS. Wanafunzi watakaopata nafasi za malazi ndani ya chuo watatakiwa kufanya malipo kupitia namba ya malipo (*control number*) itakayopatikana toka mwenye mfumo wa SARIS na kisha kuwasilisha risiti ya malipo chuoni.

Hata hivyo, kupitia **Kurugenzi ya Huduma za Wanafunzi kwa kushirikiana na Serikali ya Wanafunzi**, chuo kimethibitisha uwepo wa nyumba/hosteli kadhaa binafsi nje ya kampasi ambazo wanafunzi wanaweza kuzitumia kwa makazi wakati wa masomo yao. Wanafunzi watatakiwa kuwasiliana moja kwa moja na wasimamizi wa hosteli husika ili kuthibitisha upatikanaji wa nafasi, gharama za malazi na masharti mengine kabla ya kufanya malipo yoyote. Wanafunzi watatakiwa kuingia mkataba na wamiliki wa makazi haya binafsi na kufanya malipo moja kwa moja kwa wamiliki wa makazi. Wanafunzi wanashauriwa kuepuka kulipia gharama za makazi kwa madalali au watu wengine wa kati (*third parties*).

Hosteli Zilizothibitishwa na Mawasiliano Yake

S/N	Jina la Hosteli	Eneo	Umbali kutoka Mloganzila Campus (m)	Simu
1.	Afyatime Hostel	Mloganzila Stand	800	0789594597 / 0713308097
2.	Anastasia Hostel	Mloganzila Jeshini	800	0793104326
3.	Davis Hostel	Kwa Makyo	800	0769183438
4.	J. Minara Hostel	J. Minara Street	300	0744520422 / 0674302342
5.	Kingu Hostel	Kwa Mwaka	800	0684769065
6.	Magambo Hostel	Kwa Freemason	1,000	0682357301

7.	Rafiki Hostel	Mloganzila Madukani	1,200	0784864417
8.	Unishelter	Mloganzila Stand	500	0691855852

NB: Orodha hii si kamilifu. Wanafunzi wako huru kuingia mkataba na wamiliki hawa au wamiliki wengine watakaochagua wenyewe.

4. Wanafunzi wenye kuhitaji maelezo zaidi au msaada wowote kuhusu malipo, makazi au taratibu nyingine za kujiunga na chuo wawasiliane kupitia:

Simu: 0715 803 081 Ms.S. Mwazembe -Senior Warden
0762 377 263 Mr.A. Fereji- Warden

KARIBUNI SANA MUHAS - KAMPASI YA MLOGANZILA

Tunawatakia maandalizi mema, safari njema na mafanikio katika safari yenu ya kitaaluma.

Limetolewa na Kurugenzi ya Huduma za Wanafunzi-MUHAS

28 Oktoba 2026